JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Dk. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge, Akiwasilisha katika Bunge Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2000/2001

2000
KIMEPIGWA CHAPA NA MPIGACHAPA WA SERIKALI,
DAR ES SALAAM — TANZANIA

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI NA MADINI MHESHIMIWA DK. ABDALLAH OMARI KIGODA, MBUNGE, AKIWASILISHA KATIKA BUNGE MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KWA MWAKA 2000/2001

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea, kujadili na kisha kuidhinisha makadirio ya fedha za Maendeleo na Matumizi ya Kawaida ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2000/01.

## A: UTANGULIZI

2. **Mheshimiwa Spika,** nikupongeze kwa uongozi wako mzuri uliolifikisha Bunge hili katika kikao chake hiki cha mwisho. Niwashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, Frederick T. Sumaye (Mbunge), Waheshimiwa Nassoro W. Malocho (Mbunge), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Urekebishaji Mashirika ya Umma na Daniel N. Yona (Mbunge), Waziri wa Fedha, kwa hotuba zao. Aidha, hapa mwanzoni niwashukuru Wabunge wenzangu wote kwa mashirikiano mazuri katika kipindi chote cha Bunge hili la awamu ya tatu yaliyotuwezesha kutekeleza mengi hasa katika sekta za

Nishati na Madini na hivyo kutuwezesha kupata mafanikio makubwa.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee niwashukuru wananchi wa jimbo langu la Handeni kwa ushirikiano mzuri na imani waliyonionyesha katika kipindi chote cha Bunge hili. Wote tunaelewa Roma haikujengwa siku moja hivyo basi tuendelee na jitihada zetu za kujenga Taifa letu.

3. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 1999, Taifa lilimpoteza kiongozi wake mashuhuri, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Ulikuwa msiba mzito, lakini baba yetu ametuachia misingi madhubuti ya upendo na ushirikiano. Tuzidi kumwomba Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, Amin. Mapema mwaka huu, tulimpoteza mwanamapinduzi Alhaji Idris Abdul Wakil, Rais Mstaafu wa Zanzibar. Aidha, Bunge lako hivi karibuni limewapoteza wabunge watatu. Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, Amin.

## B: MAJUKUMU

4. **Mheshimiwa Spika,** baada ya makadirio ya mwaka 1999/2000 kupitishwa Wizara yangu iliandaa programu ya kazi na ratiba ya utekelezaji wake. Programu hiyo ndiyo iliyokuwa dira ya kutekeleza majukumu yetu.

## C: MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA 1999/2000 NA MAELEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 2000/01

5. **Mheshimiwa Spika,** uamuzi wa Serikali wa kuiruhusu Wizara kutumia sehemu ya maduhuli inayokusanya kuendeshea shughuli zake umeiwezesha kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kukusanya maduhuli zaidi na hivyo kumudu gharama za matumizi ya kawaida. Katika mwaka 2000/01 Wizara itaendelea kuimarisha ukusanyaji ili iweze kugharimia shughuli za maendeleo.

## D: SEKTA YA NISHATI

### Sekta Ndogo ya Umeme

6. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 1999 vituo vya umeme hapa nchini vilizalisha jumla ya uniti milioni 2,324.6 ikilinganishwa na uniti milioni 2,102.4 zilizozalishwa mwaka 1998.

7. **Mheshimiwa Spika, TANESCO** imekamilisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme cha Kihansi chenye uwezo wa kutoa megawati 180 na njia ya kusafirishia umeme ya msongo wa kilovoti 220 kutoka Kihansi hadi Iringa na Kihansi hadi Kidatu. Mradi huu unatarajiwa kuzinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Julai, 2000.

8. **Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha kwamba umeme unapatikana katika vituo ambavyo havikuunganishwa na gridi ya Taifa, **TANESCO** imekarabati mitambo ya umeme ya vituo vya Njombe, Sumbawanga, Bukoba, Kigoma na Mtwara. Kazi ya kufunga mitambo iliyohamishwa kutoka Musoma na Mpwapwa na kupelekwa katika vituo vya Mtwara, Kigoma na Kilwa Masoko imekamilika. Hadi sasa **TANESCO** imekwishahamisha mashine sita kutoka kituo cha Kihansi na kuzipeleka katika miji ya Lindi, Mtwara, Kigoma na Songea. Ufungaji wa mitambo hiyo utaongeza megawati moja Lindi na Mtwara na megawati mbili kwa miji ya Kigoma na Songea. Aidha, Serikali ya Norway imetoa shilingi bilioni 4.7 kwa ajili ya kuupatia umeme mji wa Sumbawanga kwa kujenga njia ya msongo wa kilovoti 66 kutoka Mbala, Zambia. Mchango wa Serikali hadi mradi huu kukamilika utakuwa shilingi milioni 330. Utekelezaji wa mradi umeanza na unategemewa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2001.

9. **Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi mahitaji ya umeme jijini Dar es Salaam, mfumo wa usambazaji umeme unapanuliwa kwa kuongeza idadi ya vituo vya kupunguza nguvu za umeme pamoja na kujenga njia mpya za usambazaji. Serikali kwa kushirikiana na Serikali za Japan na Norway zinagharimia kazi hii.

10. **Mheshimiwa Spika,** kazi ya uenezaji umeme nchini inaendelea vizuri. Kati ya miji mikuu 15 ya Wilaya iliyopangwa kupatiwa umeme, miji 13 ilikuwa imepatiwa umeme hadi mwezi Machi, 2000. Aidha, miji mingine 5 ya wilaya inatarajiwa kupatiwa umeme ifikapo mwisho wa mwaka huu na hivyo kuvuka lengo kwa miji 3 ya wilaya.

Pamoja na miji hiyo ya wilaya, miji midogo 17 na vijiji zaidi ya 330 vimepatiwa umeme katika kipindi cha 1995 hadi 2000. Wilaya ambazo zimepatiwa umeme ni Kiteto, Karatu, Mbulu, Makete, Bunda, Ileje, Ulanga, Sengerema, Mbinga, Iramba, Manyoni, Chunya na Mkuranga. Miji midogo ambayo imepatiwa umeme ni Kibaigwa, Kilwa Kivinje, Itigi, Manonga, Mto wa Mbu, Oldeani, Magugu, Dareda, Ilula, Ilembula, Maji ya Chai, Merelani, Iguguno, Kinampanda, Mkata, Manga, Galapo, Gairo na Lake Manyara. Miji inayotarajiwa kupatiwa umeme mwaka huu wa fedha ni Geita, Meatu, Igunga, Kibakwe, Tandahimba, Ruangwa, Nasa, Ngara, Biharamulo, Chato na Kanyigo. Wilaya ambazo hazijapatiwa umeme ni Ngorongoro, Simanjiro, Ludewa, Serengeti, Mbarali, Rufiji, Nkasi, Bukombe, Sikonge, Ukerewe, Kasulu na Kibondo.

11. **Mheshimiwa Spika,** kwa takwimu zilizotolewa hapo juu ni dhahiri kwamba bado tunayo kazi kubwa

mbele yetu ya kupeleka umeme kwenye maeneo mapya.
Mahitaji ya umeme yanaongezeka takriban kwa asilimia 7.9 kwa mwaka kutokana na maendeleo ya uchumi na jamii.

12. **Mheshimiwa Spika, TANESCO** inategemea mapato yatokanayo na mauzo ya umeme ili kukidhi gharama zake za uendeshaji. Hata hivyo, hali ya Shirika kifedha siyo nzuri kutokana na uhaba wa makusanyo ya madeni ya umeme. Hadi kufikia mwezi Mei, 2000 Shirika lilikuwa linadai taasisi za Serikali, Serikali yenyewe, mashirika ya umma na wateja binafsi jumla ya shilingi bilioni 75.1 zikiwa ni malimbikizo ya malipo kwa ajili ya matumizi ya umeme. Kati ya hizo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inadaiwa shilingi bilioni 17.8 na Serikali ya Muungano shilingi bilioni 33.7 (hata hivyo deni la Serikali ya Muungano limepungua hadi kufikia shilingi bilioni 30.1 baada ya Serikali kuilipa **TANESCO** shilingi bilioni 3.6 tarehe 28/6/2000). Taasisi za Umma zinadaiwa shilingi bilioni 16.5. Ucheleweshaji wa kulipwa madeni hayo kumeifanya **TANESCO** kuathirika katika kutekeleza shughuli zake na kujiendesha. Aidha, hivi sasa Shirika limeshindwa kuendelea na miradi ya umeme vijijini kutokana na uhaba wa fedha. Wakati huo huo likijitahidi kununua mafuta ya kuendeshea mitambo kadhaa ya kuzalisha umeme.

13. **Mheshimiwa Spika,** Mwezi Oktoba, 1999 Serikali iliamua kuwa muundo wa **TANESCO** urekebishwe kwa kutenganisha shughuli za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme. Hivi sasa sheria na kanuni mpya za umeme zitakazoleta ushindani na uwekezaji zaidi katika shughuli za utoaji wa huduma ya umeme zinaandaliwa. Baada ya hapo **TANESCO** ianze kubinafsishwa kwa awamu. Kufuatia uamuzi huo, hivi sasa Wizara yangu kwa kushirikiana na **PSRC** tumeunda *Divestiture Technical Team* itakayoratibu maandalizi hayo. Inatarajiwa kuwa sheria mpya ya umeme itawasilishwa Bungeni mwaka 2002, na taratibu za ubinafsishaji zitaanza mwaka 2003 au 2004. Baada ya hapo shughuli zote za uendeshaji katika sekta ya umeme zitasimamiwa na chombo maalum, *Tanzania Utility Regulatory Authority.*

14. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuwa na wajibu wa kugharimia miradi ya kupeleka umeme vijijini, kama ilivyobainishwa katika "Mwelekeo Mpya wa Sekta ya Umeme". Hivyo basi, Serikali itaanzisha Mfuko wa Umeme Vijijini, *Rural Electrification Fund,* na kutoa vivutio kwa uwekezaji vijijini pamoja na kuhamasisha uanzishaji wa vyama vya ushirika wa umeme vijijini, *Rural Electrification Co-operatives.* Ili kuiandaa sekta ya umeme kwa mageuzi ya uwekezaji na uendeshaji, sambamba na urekebishaji wa sekta ya umeme, Serikali inawasiliana na wafadhili mbalimbali ikiwemo Benki ya Dunia ili kupata fedha za kutekeleza miradi ya upanuzi wa

huduma ya umeme. Miradi hii italenga kuwapatia umeme wananchi waishio kwenye maeneo ya karibu na miji na vijijini.

### Mwelekeo Kuelekea Miaka ya 2000

15. **Mheshimiwa Spika,** kuanzia sasa ambapo shughuli za uwekezaji na uendeshaji wa biashara upo mikononi mwa sekta binafsi, utekelezaji wa majukumu ya Wizara utachukua sura mpya na kuwa tofauti. Wizara itakuwa na vyombo vya kusimamia kampuni na wawekezaji binafsi katika sekta ya nishati, *regulatory bodies,* ambavyo vitahakikisha kuwepo kwa mizania ya huduma zitolewazo na wawekezaji katika sekta kwa wateja wanaonufaika kutokana na huduma hizo.

16. **Mheshimiwa Spika,** sera ya nishati ya mwaka 1992, hivi sasa imepitwa na wakati. Wizara yangu iliamua kuidurusu ili iendane na wakati tulionao tukizingatia michango ya washitiri, Waheshimiwa Wabunge, pamoja na matakwa na hali halisi ya mazingira ya nchi yetu. Kama tulivyoandaa sera mpya ya madini, tunatarajia kuwa sera mpya ya nishati itachochea utekelezaji wa majukumu ya sekta ya nishati.

17. **Mheshimiwa Spika,** uhaba wa mvua za masika katika msimu huu umesababisha upungufu wa maji

katika mabwawa ya Mtera na Nyumba ya Mungu. Hadi kufikia mwanzoni mwa mwezi Juni, kina cha maji kwenye bwawa la Mtera kilikuwa mita 693.7, kikilinganishwa na kina cha juu cha mita 698.5 na kile cha chini cha mita 690.0. Aidha, kwenye bwawa la Nyumba ya Mungu kina cha maji kimefikia mita 685.7 kikilinganishwa na kina cha mita 687.7 wakati kama huu mwaka 1999. Hivyo, hali ya maji kwenye bwawa hili linalohifadhi maji kwa ajili ya vituo vya Hale na Pangani vile vile siyo nzuri. Shirika la Umeme, linachukua hatua za tahadhari za kuiweka mitambo ya gesi na ile ya dizeli katika hali nzuri ya uzalishaji ili isaidiane na mitambo ya maji kwa nia ya kuepuka mgao wa umeme.

**Sekta Ndogo ya Petroli na Gesi**

18. **Mheshimiwa Spika**, kuanzia Januari mosi, 2000 Serikali ilianzisha mfumo wa soko huria la biashara ya mafuta ya petroli. Kuanzishwa kwa mfumo huo kulizipa uhuru kampuni za mafuta kujipangia bei kwenye vituo kwa kuzingatia gharama halisi za upatikanaji wa mafuta katika soko la dunia. Hata hivyo, tangu tuingie katika mfumo wa soko huria, bei za mafuta zimekuwa zikipanda kwenye soko la dunia na hivyo kuathiri pia bei za mafuta nchini. Kwa mfano mwezi Februari, 2000 bei ya mafuta ya dizeli ilifikia wastani wa Dola za Marekani 226.8 kwa tani ikilinganishwa na Dola za Marekani 84.0 kipindi hicho

hicho mwaka 1999. Mwelekeo wa bei ya mafuta kwenye soko la dunia ndicho kigezo kikubwa cha kushuka au kupanda kwa bei za mafuta nchini.

19. **Mheshimiwa Spika,** kampuni ya Addax & Oryx Group Ltd, imenunua asilimia 50 ya hisa za kiwanda cha **TIPER** na Agip Tanzania Ltd kutoka kampuni ya Agip Petroli ambazo ni asilimia 50 ya hisa za kampuni hizo. Serikali kupitia **PSRC,** inaendelea na matayarisho ya kuuza hisa zake katika kampuni hizo kwa watu na kampuni binafsi.

### Utafutaji wa Mafuta

20. **Mheshimiwa Spika,** kampuni zote tulizokuwa nazo mwaka jana bado zinaendelea na utafutaji isipokuwa Gulf Western kutoka Kupros na Antrim Resources kutoka Canada. Kampuni za Canop, Dublin International, Ndovu Resources na Western Geophysical zimetumia jumla ya Dola za Marekani milioni 29.7 kwa mwaka 1999/2000 na zimepanga kutumia Dola za Marekani milioni 38.1 katika kipindi cha 2000/01.

### Majukumu ya TPDC Katika Soko Huria

21. **Mheshimiwa Spika,** majukumu ya msingi ya **TPDC** yatazingatia kuendeleza utafutaji wa mafuta na gesi asilia; kushawishi na kuvutia kampuni za utafutaji

wa mafuta; kufanya utafiti wa awali ili kuboresha kuweka, kutunza taarifa muhimu za kijiolojia na kijiofizikia za maeneo yote ya utafutaji mafuta; kuwa na leseni ya utafutaji kwa kushirikiana na kampuni nyingine kufuatana na sheria ya petroli, *Petroleum (Exploration and production)* Act, 1980 na kusimamia uzalishaji. Katika kipindi hiki cha mpito wakati Serikali inayapitia upya majukumu ya **TPDC** kabla ya kuyabadili kisheria, Shirika litategemea ruzuku kutoka Serikalini katika uendeshaji wa shughuli zake.

**Mradi wa Gesi ya Songo Songo**

22. **Mheshimiwa Spika,** mwaka jana Serikali ilitarajia kufikia makubaliano kati ya Serikali na wawekezaji pamoja na wafadhili wa mradi huu, ili utekelezaji wake uanze mwanzoni mwa mwaka 2000. Matarajio hayo hayakufikiwa kwa sababu ya umuhimu wa kudurusu baadhi ya vipengele vya mikataba, kuchuja wawekezaji kabla ya kusaini mikataba, na kutimiza wajibu wa Serikali kwa mujibu wa makubaliano na wafadhili katika miradi iliyokamilika. Matayarisho yote haya yatakamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2000 ili utekelezaji wa mradi uanze mwezi Januari, 2001.

**Mradi wa Gesi ya Mnazi Bay**

23. **Mheshimiwa Spika,** majadiliano na wawekezaji wa kampuni za *Tullow Oil* na *Cinergy* yaliyofanyika

mwezi Oktoba, 1999 hayakufikia kiwango cha kukidhi mahitaji ya Taifa katika kupeleka umeme wa gharama nafuu kwa wakazi wa mikoa ya Lindi na Mtwara. Kwa kuzingatia hilo, Serikali imeandaa mapendekezo mengine yatakayojadiliwa katika mkutano na wawekezaji utakaofanyika mwishoni mwa mwezi Julai, 2000. Hitimisho la mkutano huo, linatarajiwa kufikia makubaliano juu ya utekelezaji wa mradi au vinginevyo Serikali itatangaza upya zabuni ya kumpata mwekezaji mwenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya Taifa kabla ya mwezi Juni, 2001.

**Nishati Mbadala**

24. **Mheshimiwa Spika**, lengo la Sera ya Nishati ni kuendeleza na kuwapatia wananchi nishati za kisasa, hususan umeme badala ya kuendelea kutegemea kuni na mkaa. Hata hivyo, itachukua muda mrefu na kugharimu fedha nyingi ili kurekebisha uwiano hafifu uliopo kati ya nishati za kisasa na zile za kuni na mkaa. Wizara yangu itaendelea kuthamini mchango wa taasisi zote kwa misaada mbalimbali zinazotoa kwa ajili ya maendeleo ya Nishati Mbadala. Nishati ambazo zitaendelea kufanyiwa utafiti zaidi ni upepo, *micro-hydro,* tungamotaka (hasa majiko na matanuru sanifu ya kuzalisha mkaa) bayogesi, mionzi ya jua na makaa ya mawe.

## E: SEKTA YA MADINI

25. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Julai, 1999 sheria mpya ya madini ilianza kutumika. Matokeo yake migodi mikubwa ya kisasa inazidi kufunguliwa na kasi ya utafutaji wa madini hasa dhahabu inaongezeka kote nchini. Mgodi mkubwa wa Geita utakaozalisha tani 15.6 za dhahabu kwa mwaka ulianza uzalishaji Juni mwaka huu. Mgodi huo unamilikiwa kwa pamoja na Ashanti Goldfields na Anglogold. Huo ni mgodi wa pili mpya baada ya ule wa Golden Pride ulioanza uzalishaji mwishoni mwa mwaka 1998.

26. **Mheshimiwa Spika,** migodi mingine miwili inatarajiwa kuanza uzalishaji katika mwaka 2001 nayo ni:-

(i) Mgodi wa dhahabu wa Bulyanhulu wa kampuni ya Barrick Gold Corporation kutoka Canada utakaogharimu Dola za Marekani milioni 280 na kuzalisha tani 12.4 kwa mwaka; na

(ii) Mgodi wa North Mara wa kampuni ya Afrika Mashariki Gold Mines kutoka Australia utakaogharimu Dola za Marekani milioni 60 na kuzalisha tani 6.2 za dhahabu kwa mwaka.

27. **Mheshimiwa Spika,** mgodi mkongwe wa Williamson Diamonds Limited uliokuwa unaendeshwa kwa hasara, sasa umeimarishwa kwa kuleta mtambo mwingine, kudhibiti gharama za uzalishaji, na kufanya marudio ya kuchambua upya masalia ya mchanga uliochambuliwa miaka ya nyuma kwa teknolojia ya zamani. Uzalishaji kwa mwaka umeongezeka kutoka karati 44,492 mwaka 1995, hadi kufikia karati 234,800 mwaka 1999.

28. **Mheshimiwa Spika,** Taifa vile vile limeanza kunufaika na faida za kiuchumi na kijamii kutokana na migodi mikubwa ya Kahama Mining Corporation, Ashanti Goldfields na Anglogold, Afrika Mashariki Gold Mines pamoja na ule wa Resolute inayoanzishwa. Faida hizo ni pamoja na ada, kodi mbalimbali, mrahaba, uimarishaji wa miundombinu, huduma za maji, umeme, afya, shule, mafunzo kazini, ajira kwa wananchi na malipo kwa huduma mbalimbali zinazotolewa na kampuni za hapa nchini kwenye migodi hiyo.

29. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio yalioanza kupatikana katika sekta ya madini kwa upande mwingine yameleta changamoto. Suala moja kubwa ni mwingiliano wa matumizi ya ardhi; pamoja na udhibiti wa uharibifu wa mazingira na athari mbalimbali za kijamii zinazoweza kutokana na ongezeko la watu katika maeneo husika katika muda mfupi. Wizara imeandaa mradi unaolenga kuongeza uwezo wa

Serikali katika kusimamia na kudhibiti shughuli za madini na athari zake. Mkazo mkubwa umewekwa kwenye mafunzo kwa watumishi, uboreshaji wa mfumo wa mawasiliano, uwekaji sahihi wa takwimu; na uimarishaji wa Idara ya Madini. Mradi huu unafuatia mradi wa kuendeleza sekta ya madini nchini unaofikia mwisho wake Desemba mwaka huu na ambao unagharimiwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia.

30. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea na juhudi za kuwasaidia wachimbaji wadogo kwa kushawishi watu na kampuni binafsi kufungua maduka ya vifaa vya uchimbaji wa madini hapa nchini. Kampuni ya Flaxwal tayari imeleta vifaa nchini na inawauzia wachimbaji na ile ya Meremeta imeendelea na utaratibu wa kuwakodisha. Aidha, Wizara yangu inaendelea kuhamasisha taasisi za fedha kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wachimbaji wadogo na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu namna ya kuandaa michanganuo inayowawezesha kupata mikopo hiyo.

31. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mafunzo, Wizara yangu imeandaa *Training Manual* kuhusu uchimbaji na uchenjuaji bora wa madini na kuanzisha vituo vya mafunzo katika Wilaya ya Chunya, Tarime, Mpanda na Igunga. Wizara yangu pia inaendelea kutoa mafunzo ya uchimbaji bora na utunzaji wa mazingira kupitia mradi wa kuendeleza sekta ya madini na mradi unaofadhiliwa na **UNIDO.**

32. **Mheshimiwa Spika,** vilevile Wizara imetayarisha vijitabu, *Code of Practice,* vinavyoeleza taratibu za kupima viwanja, uchimbaji bora, hifadhi ya mazingira, matumizi ya baruti, afya ya jamii na usalama wa migodi kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Vijitabu hivi viko katika lugha ya Kiswahili na vimesambazwa kwenye ofisi zote za madini nchini ili wachimbaji wadogo waweze kuvipata kwa urahisi. Juhudi zinafanyika pia ili vianzishwe vipindi vya redio na televisheni vinavyotoa elimu juu ya uchimbaji na uzalishaji wa madini unaozingatia hifadhi ya mazingira.

**Biashara ya Madini**

33. **Mheshimiwa Spika,** mauzo ya madini nchi za nje kwa mwaka 1999 yaliongezeka karibu mara nne na kufikia Dola za Marekani milioni 80.4 kutoka Dola za Marekani zipatazo milioni 22.6 mwaka 1998. Sehemu kubwa ya ongezeko hilo imetokana na uzalishaji wa dhahabu kwenye mgodi wa Golden Pride wilayani Nzega na pia kupanda kwa uzalishaji wa almasi katika mgodi wa Williamson Diamonds Limited, Mwadui. Aidha, kumekuwepo na ongezeko la mauzo ya vito toka Dola za Marekani milioni 8.1 mwaka 1998 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 14.0 mwaka 1999. Mauzo ya madini ya *rock phosphate* iliyosagwa kutoka Minjingu yaliongezeka kutoka Dola za Marekani 20,000 mwaka 1998 hadi kufikia Dola za Marekani 230,000 mwaka 1999 kufuatia jitihada za kupanua soko la matumizi ya moja kwa moja ya madini hayo mashambani, nchini Kenya.

34. **Mheshimiwa Spika,** ingawa biashara ya vito kupitia mkondo halali imeongezeka ikilinganishwa na miaka ya nyuma, bado sehemu kubwa ya madini yetu yanauzwa nchi za nje yakiwa ghafi. Pamoja na kivutio kilichowekwa kutolipia mrahaba, kwa madini yaliyokatwa, kampuni nyingi hususan zenye ubia na wageni bado zinapeleka madini yasiyokatwa katika nchi wanakotoka. Nchi hizo ndizo zinanufaika na ongezeko la thamani na ajira kwa raia wao. Kishawishi kikubwa sio uzalendo bali tofauti ya mifumo ya kodi. Mathalan nchini India, wauzaji wa madini yaliyosanifiwa kwenda nchi za nje hawatozwi kodi ya mapato. Kulingana na utafiti uliofanyika, kodi zetu za msingi nchini Tanzania hazitofautiani sana na kodi katika nchi nyingine. Isipokuwa, tunazo kodi ndogo ndogo nyingi na isitoshe, zenye urasimu mrefu na usumbufu katika ukusanyaji wake.

35. **Mheshimiwa Spika,** mfumo wetu wa kodi ndio unaochangia kwa kiasi kikubwa utoroshaji wa madini. Kwa hiyo basi, Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Fedha kuangalia upya uwezekano wa kufuta kodi zote ndogo ndogo ili kuliletea Taifa letu mapato makubwa. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana, Uhamiaji na uongozi mikoani:

(a) wageni wanaoingia nchini wameanza kudhibitiwa; na
(b) tunatafuta wafadhili kuanzisha mafunzo ya wakufunzi *(training of*

*trainers)* ya ukataji wa vito katika vyuo vya **VETA** na vyuo vingine vya ufundi nchini.

36. **Mheshimiwa Spika**, masharti ya utoaji wa leseni za biashara ya madini kwa kampuni zenye ubia na wageni pia yanaangaliwa upya. Lengo ni kuwakaribisha wawekezaji wenye uwezo. Masharti mapya yatakayowekwa yatatangazwa katika vyombo vya habari ili kupata wawekezaji kutoka nchi mbalimbali tofauti na ilivyo sasa. Hali hiyo itaimarisha ushindani na kupunguza uwezekano wa wanunuzi kula njama na kupanga bei za chini wanaponunua madini kutoka kwa wachimbaji.

## F: USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

### Ushirikiano na Nchi za SADC

37. **Mheshimiwa Spika,** nchi yetu imeendelea kushirikiana na nchi wananchama wa **SADC** katika uendelezaji wa sekta za nishati na madini. Tanzania iliridhia itifaki ya madini kupitia Azimio la Bunge Na. 7 la mwaka 1999. Aidha, mwezi Mei, 2000 Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mkutano *wa Governing Council* ya **SEAMIC** uliofanyika jijini Dar es Salaam.

### Ushirikiano na Nchi na Mashirika ya Kimataifa

38. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukrani nyingi kwa serikali na mashirika ya kimataifa ambayo yameendelea kushirikiana nasi. Kwa niaba ya Serikali natoa shukrani za dhati kwa Serikali za Australia,

Canada, China, Denmark, Finland, Hispania, Jamhuri ya Ireland, Japan, Norway, Sweden, Ufaransa, Ujerumani na mashirika ya kimataifa yafuatayo: **ADB, CDF, DEG, EIB, EU, IFC, IMF, KFW, NDF, NORAD, SIDA, UNESCO, UNIDO, USAID na WB.**

## G: MAENDELEO YA WATUMISHI

39. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 1999/2000 Wizara yangu iliweza kuajiri watumishi wapya 9 na watumishi 12 walikoma katika utumishi wa Serikali kwa sababu kadhaa. Katika kipindi hicho Wizara iliwapandisha vyeo jumla ya watumishi 204 kati ya watumishi 490.

### Chuo cha Madini

40. **Mheshimiwa Spika,** mwaka uliopita ujenzi wa ofisi, madarasa, bweni, jiko na bwalo uliendelea vizuri. Aidha, maandalizi mengine ya kukamilisha mtaala, vifaa vya mafunzo pamoja na ununuzi wa samani yanaendelea vyema. Katika mwaka huu wa fedha Chuo kitaanza kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya ufundi mchundo.

## H: MAJUMUISHO

41. **Mheshimiwa Spika,** niishukuru Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Juma J. Akukweti, Mbunge wa Tunduru. Nawashukuru Mheshimiwa Alhaj Manju Salum Omari Msambya, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini na Naibu Waziri wa Nishati na Madini na Bwana Patrick Rutabanzibwa, Katibu Mkuu Wizara. Aidha,

ninawashukuru watumishi wote wa Wizara na mashirika yaliyo chini yake kwa ushirikiano wao katika utendaji kazi. Pia napenda kumpongeza Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kukamilisha kupiga chapa hotuba hii kwa wakati.

42. **Mheshimiwa Spika,** nawaomba waheshimiwa wabunge warejee kwenye majedwali yanayoanzia ukurasa wa **21** kwa ufafanuzi zaidi wa hotuba yangu.

43. **Mheshimiwa Spika,** sasa naliomba Bunge lako likubali na kuidhinisha mapendekezo ya Bajeti ya shilingi 38,375,044,500 kwa ajili ya Wizara na mashirika yake kwa kipindi cha 2000/01. Mchanganuo wa bajeti hii ni kama ifuatavyo:-

Bajeti ya maendeleo ni shilingi 35,362,000,000 ambazo kati yake shilingi 6,362,000,000 ni fedha za hapa na shilingi 29,000,000,000 ni fedha za nje. Aidha, Bajeti ya Matumizi ya kawaida ni shilingi 3,013,044,500.

44. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**MAJEDWALI NA MICHORO**

**WILAYA NA VIJIJI VILIVYOPATIWA UMEME KATI YA JUNI 1999 NA MEI 2000 NA VINAVYOTARAJIWA KUPATIWA UMEME KABLA YA MWISHO WA JUNI, 2001**

| **Mkoa/Wilaya** | **Vijiji Vilivyopata umeme Juni 1999 hadi Mei 2000** | **Vijiji vitakavyopatiwa umeme kabla ya Juni, 2001** |
|---|---|---|
| **Mkoa wa Mbeya** | | |
| 1. Mbeya Vijijini | Inyala, Simambwe,Galijembe, Izumbwe,Lwambi,Mtakuja, Nsalala, Isitu, Ituha na Ihombo | Kawetere,Lwalanje,Isyenye, Ijombe |
| 2. Rungwe | Mpanda, Lufilyo, Itete,Ibula, Lugombo,Mwakaleli | Mbigiri,Mpombo,Ngopyolo, Mbeyache, Lugombo-Iponjola |
| 3. Mbozi | IlemboMjengo,Luanda, Kilimapimbi | Mahenge,Malonje |
| 4. Chunya | Saza, Matungasi,Mkola | Mwambani |
| 5. Ileje | Msia | |
| 6. Kyela | | Ipinda, Ipyana,Tenende, Nkuyu, Ndandalo,Talatala, Bujonde. |
| **Mkoa wa Kagera** | | |
| 7. Bukoba Vijijini | Kashenye,Bunazi | Kanyigo,Katerero Chuo cha ELCT |
| 8. Karagwe | Ndama | |
| 9. Muleba | Kishoju Secondari,Katoke,Igabiro | |
| **Mkoa wa Iringa** | | |
| 10. Iringa Vijijini | Migori,Mawerewere, Lundamatwe, Mangalali, Ilula, Isele, Itunda | Ilula Ilala, Mbigiri, Magubike |
| 11. Mafinga | Luganga | Nyololo, Kinyanambo |
| 12. Njombe | Mtwango Sekondari, | Wangama, Ikelu, Luponde,Mtwango,Mlata, Kihesa |
| 13. Makete | Kikondo | Mongolo |
| **Mkoa wa Tanga** | | |
| 14. Tanga Vijijini | Mabokweni,Horohoro, Kwakaeza Kwanjeka, Donge, Kange | |
| | | |
| 15. Muheza | Misozwe, Genge | Bombani, Enzi, Nkumbu |

| | | |
|---|---|---|
| 16. Korogwe | Segera Mashine,Segera Njia Panda | Lewa, Mkumbulu, Mashewa |
| 17. Lushoto | Mlalo Mlalo Mission, Ngulwi,Funta, Mbuzi,Malindi Nyasa, Majulai, Moa. Dule, Chambageni, Ndekoi, Mnadani | |
| 18. Handeni | Mkata, Kwenjugo, Kitumbi 'A', Kitumbi 'B', Manga | Kwemkonga, Kwachaga, Mazingara, Sua, Msento, Mkuyu Mafleta, Mswaki, Kwediboma |
| 19. Pangani | Mkwaja | Kipumbwi |
| **Mkoa wa Mtwara** | | |
| 20. Masasi | Chikukwe, Lupaso, Chikundi, Lukuleli | Chidya, Mkalapa, Chigugu |
| 21. Newala | Lufindi | Makonga |
| 22. Tandahimba | | Tandahimba, Nanyanga |
| **Mkoa wa Lindi** | | |
| 23. Lindi Vijijini | Nyangao vijijini, Nyangao Hospital, Machumbika | |
| 24. Kilwa | Kilwa | |
| 25. Nachingwea | Naipange | Ndomoni |
| 26. Ruangwa | | Ruangwa, Likunja,Mkowe |
| **Mkoa wa Dodoma** | | |
| 27. Kondoa | Bioha,Maji ya Shamba, Kwantisi Wigi, Bolisa,Kimani,Aya Sekondari Mondo, Kelema Maziwani, Songolo, Chandama, Mrijo Juu, Mrijo Chini | |
| 28. Kongwa | Kongwa Ranch, Narco Kongwa,Gairo | |
| 29. Dodoma Vijijini | Ihumwa, Mdemu Nyuka, Mkonze, Kibaigwa | |
| 30. Mpwapwa | | Kibakwe |
| **Mkoa Morogoro** | | |
| 31. Morogoro Vijijini | Mlali, Kauzeni, Kigugu,Village,Manyinga, Area, Kigurunyembe, Kihonda Block 'F' Sekondari, Kichangani Area B, Kichangani, Lusanga | Dark City Mafisa |
| 32. Kilosa | Mamoyo,Muungano Village | Parakuyo, Kondoa Kitete |
| 33. Mahenge | Mahenge,Kichangani, | |

| | | |
|---|---|---|
| | Mavimba, Milola,Watoto yatima | |
| 34. Ifakara | Kivukoni,Mlimba,Kilwarila, Tangani,Upangala,Nawenge Block O | |
| 35. Kilombero | Mkula | Kitete,Mikumi Sekondari, Sumbugulu |
| **Mkoa wa Arusha** | | |
| 36. Arusha Vijijini | Nambere,Village,Emaoi, Moivaro, Engosangia,Mukurati, Kivululu | |
| 37. Usa River | Ngyani, Ulonoa, Nguruma,Mulala, Akheri Kati,Sakila,Dam Akeri,Shimbumbu,Akheri, Maji ya Chai, Ndoombo. | |
| 38. Monduli | Ngarash,Mlimani, Lashaine,Kisongo | |
| 39. Mererani | | Mbuguni |
| 40. Babati | Galapo,Dareda,Kiru,Babati Vijijini (Nakwa,Mrara juu,Hangoni) | Mapea |
| 41. Karatu | Mji wa Karatu, Oldean, Ngorongoro Gate,Mto wa Mbu, Manyara | |
| 42. Mbulu | Mji wa Mbulu na vitongoji vyake | |
| 43. Kiteto | Mji wa Kibaya, Njoro | |
| **Mkoa wa Singida** | | |
| 44. Hanang | | |
| 45. Kiomboi | Kiomboi, Mara,Msingiri, Ulamo, Kinampanda | Shelui, Ndago |
| 46. Manyoni | Manyoni, Sanjaranda, Itigi | |
| **Mkoa wa Kigoma** | | |
| 47. Kigoma Vijijini | Kamala | Masanga |
| **Mkoa wa Mwanza** | | |
| 48. Magu | | Nassa, Bulima, Nyashimo, Nyang'nanga,Masanza Kona |
| 49. Geita | | Geita Mjini,Kasamwa |
| 50. Mwanza Vijijini | Nyang'holongo | |
| **Mkoa wa Shinyanga** | | |
| 51. Bariadi | Mwamapalala, Kidulya | Nyamalapa |
| 52. Shinyanga | Kishapu | Samuye |

| | | |
|---|---|---|
| Vijijini | | |
| 53. Meatu | | Gula, Sanga Mwalugesha, Sanga Hinge, Mwamishari, Mwanhuzi Mjini |
| 54. Maswa | | Sayu Sayu, Njia Panda,Ngegemo, Malita |
| 55. Kahama | | Itogwanholo |
| **Mkoa wa Kilimanjaro** | | |
| 56. Moshi Vijijini | Uru Shimbw, Materuni, Yam Makaa Chekereni | Kirua Vunjo Juu |
| 57. Same | Gonjanza,Ndolwa,Haikonti, Kilindini,Kitamuri, Weruweru, Gwang'a | |
| 58. Rombo | Kiraeni, Mshima,Shimbi Mashami,Mahorosho,Cosata, Keiyo, Losanga,Nangara,Nayeme, Mtimbao, Kitasha | Kyerio, Olele Chini |
| 59. Marangu | Mwika,Kirimeni, Kondeni, Lole Chini, Mshiri | Legho |
| 60. Mwanga | Kisangara Juu, Kisangiro,Kileo, Njia Panda Kilomeni | Mlevo |
| 61. Hai | Mashua, Suti, Kwamarali,Kyengia Sawe | |
| **Mkoa wa Tabora** | | |
| 62. Nzega | Mwakuzuge,Nzogooo, Tezengwa Kilini, Isanga | |
| 63. Igunga | Manonga Ginnery, Choma cha nkola Ziba Nanga | Igunga Mjini, Igunga Vijijini |
| 64. Tabora Vijijini | Kiluni | |
| **Mkoa wa Mara** | | |
| 65. Musoma Vijijini | Ikizu,Bitirio, Muhendwe, Ruhu | |
| 66. Bunda | Bunda mjini, Guta Pumps | |
| **Mkoa wa Pwani** | | |
| 67. Mkuranga | Mwandege,Mkuranga Mjini, Vikindu, Kisanawale | Vitongoji vya Mkuranga Mjini |
| 68. Kibaha | Kiluvya, Nyumbe, Pangani Mitambani, Soga | |
| 69. Bagamoyo | Miligotini, Mandera Ruvu | |
| 70. Kisarawe | Sungura, Mikongeni, Pugu, Kigogo, Majinde, Mashariki, Kinyamwezini | |

| **Mkoa wa Dar es Salaam** | | |
|---|---|---|
| 71. Temeke | Tungi, Kongowe, Buza | |
| 72. Kinondoni | Tegeta, Tandale, Kawe Darajani, Madale, Youth, Kisauka,Boko (JKT), Salasala, Teta, Mbweni, Goba Juu Ndimbwi, Magone, Tegeta Nyatini | |
| 73. Ilala | Kinyerezi Kipunguni, Kitunda, Magola, Ndege, Kisukuru Juu. | |

**UZALISHAJI WA UMEME 1992 - 1999 (khw '000,000')**

| AINA YA UMEME | MWAKA | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1992 | 1993 | 1994 | 1995 | 1996 | 1997 | 1998 | 1999 |
| HYDRO | 1649.00 | 1796.66 | 1499.38 | 1538.78 | 1747.76 | 1449.16 | 2077.62 | 2,164.5 |
| THERMAL | 269.34 | 180.81 | 293.15 | 309.74 | 211.30 | 485.00 | 24.79 | 160.1 |
| KUTOKA NJE | - | - | - | 32.38 | 32.73 | 44.00 | 45.04 | 53.3 |
| JUMLA | 1918.34 | 1977.47 | 1792.53 | 1880.89 | 1991.79 | 1978.16 | 2147.45 | 2,377.9 |

Chanzo: TANESCO

**MATUMIZI YA UMEME 1993 – 1999 KATIKA ASILIMIA**


| AINA YA WATUMIAJI | MWAKA | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1993 | 1994 | 1995 | 1996 | 1997 | 1998 | 1999 |
| General (T1) | 54.20 | 56.49 | 54.33 | 59.85 | 58 | 59 | 56.0 |
| Low voltage (T2) | 8.70 | 9.63 | 4.16 | 16.76 | 18 | 16 | 13.0 |
| High voltage (T3) | 33.20 | 29.29 | 31.70 | 18.37 | 19 | 18.90 | 23.4 |
| Public Light (T4) | 0.80 | 0.90 | 0.62. | 0.18 | 1 | 0.10 | 0.5 |
| Bulk Sales (T5) | 3.10 | 3.69 | 5.08 | 4.84 | 4 | 6.0 | 7.1 |
| Jumla | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.0 |


Chanzo: TANESCO

T1 –T5 – Tariff group


# MINERAL EXPORTS 1994 - 1999

| | | 1994 | | 1995 | | 1996 | | 1997 | | 1998 | | 1999 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mineral type | Unit | Weight | Value (Mill.US$) | Weight | Value (Mill.US$) | Weight | Value (Mill.US$) | Weight | Value (Mill.US$) | Weight | Value (Mill.US$) | Weight | Value (Mill.US$) |
| Diamonds | Carats | 22,567 | 2.9 | 44,492 | 4.34 | 126,670 | 15.47 | 123,090 | 16.59 | 95,337 | 11.11 | 234,800 | 26.37 |
| Gold | kg | 2,802 | 27.39 | 322 | 3.29 | 301 | 2.78 | 232 | 2.00 | 427 | 3.34 | 4,890 | 39.76 |
| Gemstones | Kg | 48,507 | 6.46 | 94,296 | 7.28 | 89,555 | 9.87 | 59,590 | 7.95 | 48,518 | 8.13 | 95,200 | 14.04 |
| Salt | Tonnes | 1,596 | 0.1 | - | - | 143,331 | 1.20 | 1,030 | 0.06 | - | - | - | - |
| Tin | Tonnes | 6 | 0.018 | 3 | 0.00 | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Graphite | Tonnes | 0 | 0 | 100 | 0.09 | 163 | 0.12 | 1,465 | 0.80 | - | - | - | - |
| Gypsum | Tonnes | 400 | 0.003 | 500 | 0.01 | 30 | 0.00 | - | - | - | - | - | - |
| Phosphate | Tonnes | 0 | 0 | 1,149 | 0.04 | 235 | 0.01 | 2,120 | 0.07 | 600 | 0.02 | 7,250 | 0.23 |
| Total (Million US $) | | | 36.871 | | 14.95 | | 29.45 | | 27.46 | | 22.60 | | 80.40 |



MINERAL EXPORTS 1981-1999
Value (US $)
90000000
80000000
70000000
60000000
50000000
40000000
30000000
20000000
10000000
0
1981
1982
1983
1984
1985
1986
1987
1988
1989
1990
1991
1992
1993
1994
1995
1996
1997
1998
1999
Year


LESENI ZA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI MKUBWA WA MADINI 1990 - 2000
Idadi
Mwaka
400
350
300
250
200
150
100
50
0
1990
1991
1992
1993
1994
1995
1996
1997
1998
1999
2000
9
2
18
7
11
72
9
10
59
4
30
132
1
13
100
40
192
5
21
351
13
57
321
11
23
218
11
0
68
18
Reconnaissance
Prospecting
Mining

LESENI ZA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI MADINI MKUBWA ZILIZOTOLEWA KWA KUFUATA AINA YA MADINI 1990-2000



GEMSTONES EXPORT 1981 - 1999




| | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 | 1988 | 1989 | 1990 | 1991 | 1992 | 1993 | 1994 | 1995 | 1996 | 1997 | 1998 | 1999 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Export value (US $) | 90000 | 70000 | 60000 | 60000 | 150000 | 560000 | 120000 | 160000 | 784063 | 1584673 | 1759132 | 3236700 | 3910000 | 6460000 | 7280000 | 9870000 | 7944806 | 8127248.8 | 14038767 |

Year

## MINERALS PRODUCTION 1994 - 1999

| Mineral type | Unit | 1994 | 1995 | 1996 | 1997 | 1998 | 1999 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Weight | Weight | Weight | Weight | Weight | Weight |
| Diamonds | Carats | 25,540 | 49,538 | 126,670 | 123,090 | 97,830 | 234,800 |
| Gold | kg | 2,861 | 320 | 318 | 232 | 427 | 4,890 |
| Gemstones | Kg | 48,507 | 111,404 | 142,160 | 509,489 | 48,518 | 95,200 |
| Phosphate | Tonnes | - | 6,686 | 717 | 2,120 | 1,437 | 7,250 |
| Coal | Tonnes | 45,027 | 43,200 | 52,000 | 28,443 | 45,073 | 75,044 |
| Limestone | Tonnes | 1,740,000 | 1,062,081 | 1,200,000 | - | 1,181,233 00 | 1,241,155 |
| Kaolin | Tonnes | 541 | 596 | 1,332 | 898 | - | - |
| Gypsum | Tonnes | 53,000 | 42,000 | 55,430 | 46,320 | 59,066 | 21,195 |
| Salt | Tonnes | 84,289 | 105,000 | 86,700 | 72,511 | 75,000 | 35,893 |
| Pozzolana | Tonnes | - | - | - | - | - | 2,274 |